# KIFUA KIKUU NA UNYANYAPAA




eannaso

NTLP NATIONAL TUBERCULOSIS & LEPROSY PROGRAMME

Tanzania TB Community Network

Stop TB Partnership hosted by UNOPS

## UTANGULIZI

Kifua Kikuu bado ni changamoto ya afya ya watu ulimwenguni kote na kwa Tanzania. Nchini Tanzania, inakadiriwa watu 142,000 walipata Kifua Kikuu Mwaka 2018. Kati yao, watu 75,000 tu ndio walipimwa na waligunduliwa kuwa na maambukizi. Takriban asilimia 40% ya watu waliokadiriwa kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu nchini Tanzania Mwaka 2018 hawakupimwa na kugunduliwa kuwa na maambukizi na hivyo kusababisha hatari kubwa ya kuambukiza wanafamilia, marafiki, na wanajamii wengine. Mojawapo ya sababu kubwa zilizosababisha watu hao kutopata huduma za upimaji wa Kifua Kikuu ni unyanyapaa kwa watu wenye Kifua Kikuu. Unyanyapaa huwajengea watu hofu ya kuachwa na familia, kutalikiwa na mume au mke (mwenza), kubaguliwa na jamii, kupoteza kazi, au kufukuzwa katika makaazi yao waliokodi. Kuenea kwa unyanyapaa kwa watu wenye Kifua Kikuu kunachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewa kwa upimaji na kugundulika na kuathiri utaratibu wa matibabu. Ingawa inatambulika kuwa kuna unyanyapaa unaohusiana na Kifua Kikuu, hatua kushughulikia unyanyapaa kwa watu walioko hatarini kupata Kifua Kikuu hazijitoshelezi.



## NINI MAANA YA UNYANYAPAA?

Unyanyapaa unaweza kufafanuliwa kama ishara ya aibu, fedheha, au kutokukubalika, jambo ambalo husababisha mtu kukataliwa, kutengwa, na kubaguliwa kushiriki mambo mbali mbali ya kijamii.

Unyanyapaa unaweza kufafanuliwa kama ishara ya aibu, fedheha, au kutokukubalika, jambo ambalo husababisha mtu kukataliwa, kutengwa, na kubaguliwa kushiriki mambo mbali mbali ya kijamii.

## KWANINI WATU WENYE KIFUA KIKUU WANANYANYAPALIWA?

- Watu/jamii kutokuwa na ufahamu wa jumla na uelewa wa kifua kikuu
- Kuwa na Kifua Kikuu kunachukuliwa kama ishara ya kuwa na VVU au Korona.
- Jamii zinaweza kuamini kuwa watu wenye Kifua Kikuu wameambukizwa kwa kuwa wamefanya kitu hatarishi
- Kuwa na taarifa zisizo sahihi na kutokuwa na ufahamu kuhusu namna Kifua Kikuu kinaambukizwa
- Kutojua kwamba Kifua Kikuu kinatibika.
- Taarifa potofu kwamba wanaopata Kifua Kikuu ni watu wenye utapia mlo, masikini, lishe duni na jamii ya tabaka la chini.

## UNYANYAPAA NI MAISHA HALISI UKWA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU

Unyanyapaa unatokea katika ngazi mbalimbali. Unyanyapaa unaweza kufanywa na:

- Jamii Husika
- Watu Wa Karibu Wanaokuzunguka Kwenye Jamii

NA TAASISI (ikijumuisha watoa huduma za afya )

PIA MTU ANAWEZA KUJIN-YANYAPAA MWENYEWE (unyanyapaa unaofanywa na mtu mwenye Kifua Kikuu)

Unyanyapaa pia umeenea majumbani, katika maeneo ya kazi, kwenye sehemu za ibada, na katika vituo vya afya. Ijapokuwa Kifua Kikuu kimeenea zaidi kwa wanaume, unyanyapaa unaonekana kutokea zaidi kwa wanawake, na wale ambao hawana elimu ya kutosha, na pia kwa idadi kubwa ya watu walio katika mazingira magumu wakiwemo wale wanaoishi katika makazi duni.

Unyanyapaa unaweza kuenezwa kwa hofu ya ugonjwa huo katika jamii, ambapo taarifa zisizo sahihi kuhusu Kifua Kikuu zimeenea. Familia, marafiki, na walezi wanaweza kupata unyanyapaa kwa kujihusisha na mgonjwa wa Kifua Kikuu. Majumbani, wanafamilia huogopa kushiriki vyombo na mtu aliye na kifua kikuu ingawa Kifua Kikuu kinasambazwa pale tu mtu mwenye maambukizi atakohoa, kupiga chafya, kutema mate, au kucheka na matone ya yavutwe na mtu aliyeko karibu naye, na sio kwa kushirikiana vyombo.

Kwenye maeneo ya kazi, waajiri wengine huwasimamisha kazi watu walioambukizwa Kifua Kikuu hata pale ambapo wamesha pata matibabu kwa wiki mbili, au wamekamilisha matibabu kwa miezi sita na hawawezi kuambukiza tena. Watu waliopona Kifua Kikuu wamenyimwa hati za kusafiria (viza) hata kama hawawezi kuambukiza tena. Kuendelea kutoa elimu ya Kifua Kikuu na kuondoa taarifa zisizo sahahihi kunaweza kumaliza matendo haya ya kibaguzi.

## AINA ZA UNYANYAPAA/UNYANYAPAA UNATOKEA VIPI?

Unyanyapaa unaweza kua:

- Hali ya kutarajia kuwa utanyanyapaliwa
- Kufanyiwa unyanyapaa
- Kujinyanyapaa mwenyewe



## MADHARA YA UNYANYAPAA

**KIAFYA:** Unyanyapaa, iwe ni wa kuonekana, kuzoeleka kufanywa, au wa mtu binafsi, husababisha kujitenga na kuathiri afya ya akili kwa wagonjwa wenye kifua kikuu, jambo ambalo huchangia kwa kiasi kikubwa mateso yanayotokana na kifua kikuu.

**KATIKA UTAFUTAJI WA MATIBABU:** Unyanyapaa husababisha mtu kuchelewa kutafuta huduma za upimaji na kutowakinga wengine wasipate maambukizi.

**USHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KIJAMII:** Kwa wanaume athari kubwa ya unyanyapaa ni kwenye kazi zao za kuingiza kipato. Kwa wanawake, pamoja na kuathiri kipato chao, kuna wasiwasi kwamba unyanyapaa utaathiri vibaya matarajio yao ya ndoa na uhusiano wa kifamilia.

**KWA MAKUNDI YA WATU WALIO MAZINGIRA HATARISHI:** Makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi na hatari ya kubaguliwa ni pamoja na watu wanaoishi na VVU, wafungwa, wachimbaji migodini, wakimbizi, watumiaji wa dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na wanaojidunga dawa kwa kutumia sindano, watu wanaoishi katika mazingira yasiyo rasmi, watu wenye ugonjwa wa kisukari, watoto, wazee, wahudumu wa afya, wavuvi na waganga wa jadi wako kwenye hatari kubwa ya unyanyapaa, ambayo inazidisha mazingira hatarishi kwao.

## KUTOKOMEZA KUFUA KIKUU NI JUKUMU LA KILA MTU

Kukomesha unyanyapaa kunahitaji kutumia njia mbalimbali zinazolenga afya ya mwili, akili, kijamii, kiroho, n.k. kwa wale walio na Kifua Kikuu, waathirika waliopona kifua kikuu, watafiti, wahudumu wa afya, mashirika ya kiraia, watunga sera, wafadhili, na umma kwa jumla. Kila mtu ana jukumu analohitaji kulitimiza;

Watu wenye Kifua Kikuu na Waliopona za Kifua Kikuu wanapaswa kuwa mstari wa mbele kukomesha unyanyapaa. Wanaweza kueleza uzoefu wao na changamoto zilizoko kwenye jamii ya watu wenye Kifua kikuu na kutumia watu waliopona Kifua Kikuu pamoja na kutumia mitandao au majukwaa mbalimbali.

Wahudumu wa Afya wanaweza kutoa msaada wa kisaikolojia na kutoa taarifa sahihi kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu na wasaidizi wao wa matibabu. Hii itapunguza hofu na kuzuia maambukizi.

Vikundi vya Kijamii, watu wenye ushawishi mkubwa, na asasi za kiraia zinaweza kuelimisha jamii kuhusu unyanyapaa kupitia kampeni za uhamasishaji na mazungumzo ya jamii ambapo watu walioathiriwa na Kifua Kikuu hushiriki kutoa uzoefu.

Watafiti wanaweza kuandaa au kutumia zana zilizopo kufanya tafiti kuhusu unyanyapaa unaohusiana na Kifua kikuu na kutoa matokeo kwa watekelezaji na watunga sera ili kutumia matokeo hayo katika kutunga sera zitakazokomesha unyanyapaa.

Watunga sera wanaweza kutumia matokeo ya tafiti hapo juu kubuni sera na sheria zinazolenda kuondoa unyanyapaa.

Wafadhili wafanye kazi kwa kushirikiana na Mpango wa Kitaifa wa kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma na wadau ili kuhakikisha ufadhili na utekelezaji wa afua zinazolenga kutokomeza unyanyapaa unaohusiana na Kifua Kikuu.

Idara ya Afya ya Umma ina jukumu muhimu katika udhibiti wa Kifua Kikuu kupitia utoaji wa taarifa za msingi kuhusu afya ya jamii na mikakati ya kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu.

Jamii nzima inaweza kusambaza zaidi taarifa zinazohusu Kifua Kikuu zinazotolewa kupitia vyombo vya habari ili kuwaelimisha watu wengine na kuongeza uelewa juu ya Kifua Kikuu.

## KUACHA UNYANYAPAA ILI KUTOKOMEZA KIFUA KIKUU

Unyanyapaa hushusha hari ya watu kupima huduma za upimaji, matibabu na uzingatiaji wa matibabu ya Kifua Kikuu, na mara nyingi huwafanya watu wasirudi kwenye vituo vya huduma, jambo ambalo husabisha kutokea kwa maambukizi mapya. Ni muhimu kuongeza upatikanaji wa dawa za Kifua Kikuu, kubuni vifaa vipya vya upimaji, na kuwashirikisha wahudumu wa afya katika kuzuia, kutoa huduma, lakini hivi pekee havitoshi kumaliza tatizo;

- Utafiti Zaidi unahitajika ili kuelewa namna gani unyanyapaa unaathiri mafanikio ya matibabu na kuelewa ni hatua gani zitasaidia kupunguza unyanyapaa kwenye jamii na kwenye vituo vya afya.
- Kutumia zana za kuchunguza na kubaini unyanyapaa kunaweza kusaidia kupata taarifa zitakazo saidia kuchukua hatua za kutokomeza unyanyapaa.
- Hatua za kuondoa unyanyapaa zinahitaji kuzingatia na kugusa maeneo mbalimbali ambayo unyanyapaa unaweza kutokea.
- Kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu kwa watu wenye Kifua Kikuu ni muhimu katika jitihada za kutokomeza Kifua Kikuu.
- Kutafuta watu wanaohisiwa kuambukizwa Kifua Kikuu, kama vile waliokaa karibu na mgonjwa wa Kifua Kikuu na kuhakikisha kwamba hakuna unyanyapaa wowote unaohusiana na Kifua Kikuu, pamoja na kuzingatia usawa wa kijinsia na haki za binaadamu, na ushahidi kama inavyoelezwa kwenye sera na programu mbalimbali katika kuwatafuta watu wanaohisiwa kumbukizwa Kifua Kikuu.

## MAREJEO


- Ripoti ya Kifua Kikuu iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani Mwaka 2019 (WHO Global TB Report 2019) - https://www.who.int/tb/publications/global_report/en/
- Ripoti ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi ulioandaliwa na UN (UN High Level Meeting Political Declaration on the Fight against TB) - http://www.stoptb.org/
- Azimio la haki za watu walioathiriwa na Kifua Kikuu (Declaration of the rights of people affected by tuberculosis) - http://www.stoptb.org/
- Stigma Assessment Handbook – Stop TB partnership - http://www.stoptb.org/
- Ripoti ya Kifua Kikuu na Unyanyapaa – Waharakati wa Kimataifa dhidi ya Kifua Kikuu (Factsheet: Tuberculosis and stigma – Global Coalition of TB Activist) - http://gctacommunity.org/
- Wanawake na Unyanyapaa - Waharakati wa Kimataifa dhidi ya Kifua Kikuu (Women and Stigma – Global Coalition of TB Activist) - http://gctacommunity.org/
- Watoto na Unyanyapaa - Waharakati wa Kimataifa dhidi ya Kifua Kikuu (Childhood and Stigma – Global Coalition of TB Activist) - http://gctacommunity.org/
- Wanaume na Unyanyapaa (Men and Stigma – Global Coalition of TB Activist) - http://gctacommunity.org/

# NOTES

## WASILIANA NA NASI

Tanzania TB Community Network (TTCN)

Hosted by EANNASO

Plot # 1 Olorien, Kijenge | Off Njiro Road

P.O Box 6187 | Arusha, Tanzania

+255 739 210598 ttcn.tanzania@gmail.com ttcntanzania


END TB

Tanzania TB Community Network